Tuzo ya Asasi Bora 2008
FOMU YA MAOMBI

Maelezo Juu ya Asasi		
Jina la Asasi		
Aina ya Ruzuku		Jumla ya Fedha
Lini Ruzuku ilianza		
Lini Mradi unamalizika		
Barua pepe		
Simu		
Simu ya Kiganjani		
Nukushi (faksi)		
Anuwani		
Je mnayo katiba iliyoandikwa	☐ Ndiyo	☐ Hapana
Je mnao mpango mkakati	☐ Ndiyo	☐ Hapana
Mtu wa kuwasiliana naye	☐ Ke	☐ Me
Jina Lake		
Cheo Chake		
Barua pepe		
Simu		
Habari Nyingine Kuhusu Asasi		
Dira (vision)		
Malengo (mission)		
Nani anafanya maamuzi ndani ya asasi		
Wafanyakazi na nyadhifa zao		

The Foundation for Civil Society –Tuzo ya Asasi Bora 2008

	Eneo la Tathmini	Maelezo na Mifano halisi
1.0	**Ubunifu wa kipekee na Matokeo (Mafanikio) yaliyofikiwa katika kuchochea mabadiliko kwa jamii** **(Angalia: Lazima mabadiliko yawe yameletwa kwa juhudi za pamoja za kiasasi kuliko asasi moja pekee**	**Max. Alama 30**
1.	Juhudi za AZAKi zimeonesha mabadiliko ya wazi kwa walengwa ikilinganishwa na taarifa za awali kabla ya mradi (kama zilikuwepo)	
2.	Wadau wa AZAKi wanahisi kwa kiasi kikubwa kwamba mradi umekuwa ni wa manufaa na umeongeza thamani ambapo hakuna mdau yoyote aliyewahi kuyafikia matokeo hayo kabla.	
3.	Faida za mradi zinaonekana zaidi kuwafikia masikini na yale makundi yanayotengwa na jamii wakiwemo watu wenye ulemavu, wenye kuishi na VVU/UKIMWI, Wanawake na Watoto na watu wa vijijini.	
4.	Takriban wanufaika wengi wa miradi ya AZAKi huonesha hali ya matumaini na muamko wa huduma na kazi zetu kwao.	
5.	Mabadiliko yanayochochewa na miradi ya AZAKi huzingatia masuala mtambuka kama vile VVU/UKIMWI, ulingano wa kijinsia na uendelevu wa kimazingira.	
	Alama {a/25 X 30}	

2.0	**Uwezekano mkubwa wa uendelevu wa mradi kutokana na ushirikishwaji na umiliki wa jamii**	**Max. Alama 10 na mifano halisi**
1.	AZAKi yetu inao mkakati imara wa uendelevu wa nyenzo kwa kuwa na mbadala wa vianzo vyengine vya fedha ukitoa washirika wa maendeleo (Vianzo vingi vya fedha vile vile ni dalili ya uendelevu kifedha)	
2.	AZAKi yetu imeweza kupata raslimali za vifaa na fedha kutoka bajeti za serikalini (Serikali kuu na za Mitaa) kwa ajili ya kutekeleza baadhi ya shughuli /kazi zetu.	
3.	AZAKi yetu imeanzisha mahusiano na mashirikiano na wadau wa ndani ya nchi kama ni njia ya kupunguza utegemezi wa wafadhili wa nje (Hii itakuwa ni hivyo kama mahusiano na wadau wa ndani ni kwa ajili ya kutafuta fedha)	
4.	Mashirika na Idara za Serikali katika ngazi ya Kimtaa na Kitaifa wameunga mkono juhudi zetu na wanaelekea kuziingiza katika mipango yao, bajeti na vipaumbele vyao.	
5.	AZAKi yetu ni mwanachama na hushiriki kikamilifu katika kazi za mitandao mbali mbali inayoendeleza malengo yanayofanana na dira na dhamira yetu.	
6.	Sera na taratibu zetu zimeweka na kufafanua taratibu nzuri za uendeshaji zinazoruhusu ushirikishwaji wa wanufaika wetu katika utoaji wa maamuzi katika ngazi mbali mbali za AZAKi na katika kusimamia kazi za mradi kwa jamii.	
	Alama {a/30X10}	

3.0	**Mitandao thabiti, yenye nguvu na uimarishaji wa ushirikiano kwa ajili ya kuleta matokeo.**	**Max: Alama 10 na mifano halisi**
1.	Umma (Jamii) inao mtizamo chanya juu ya AZAKi yetu na inatambua mchango wa huduma tunazozitoa.	
2.	Jamii zinazotunguzuuka na umma kwa ujumla wanaunga mkono kazi zetu na wako tayari kuzilinda ikiwa kutakuwa na haja ya kufanya hivyo	
3.	AZAKi yetu inaweza kupata taarifa na takwimu kwa urahisi zinazohusu sera, mipango, bajeti nk kutoka Idara za serikali. Mara nyingi taarifa hizi hutumika kuchochea mijadala na kushawishi watu.	
4.	Idara za serikali hutafuta mashirikiano kutoka kwa AZAKi yetu katika shughuli zake mbali mbali za maendeleo na mara nyingi huwahusisha AZAKi katika hatua zote za utekelezaji.	
5.	AZAKi imeanzisha mahusiano mema ya kazi na mashirika ya fedha ya ndani ikiwemo sekta binafsi ya ndani na kimataifa. Mahusiano haya yamejengwa kwa msingi wa uwazi na kuaminiana.	
6.	Umoja na Mitandao ya AZAKi na wadau wengine imepelekea kufikiwa kwa mafanikio na malengo ya pamoja.	
	Alama {a/30 X 10}	

4.0	**Utawala na Usimamizi**	**Max. Alama 30 and**
1.	AZAKi yetu inalo eneo la utekelazaji au wanachama	
2.	Katiba yetu, sera zetu za msingi na vitabu vya mahesabu na miongozo yetu ni rahisi kuiona na kifikiwa na wanachama na wadau wengine. Nyaraka hizi hufanyiwa marekebisho ili ziendane na wakati.	
3.	AZAKi yetu inacho chombo cha utawala (Bodi au Kamati Tendaji) ambayo imechaguliwa kwa mujibu wa taratibu zinazokubalika (Angalia muda wa uongozi na kama wanachama wametosheka na matokeo)	
4.	Muundo wa AZAKi yetu unaeleweka vizuri na wafanyakazi, wanachama, Bodi / Kamati Tendaji	
5.	Muundo unaonesha kwa uwazi mfumo wa mawasiliano, uwajibikaji na kukasimu madaraka ya uendeshaji na usimamizi kati ya uongozi na utawala.	
6.	Angalu theluthi moja ya wajumbe wa Bodi wanao utaalamu unaohitajika kuendeleza dhamira kuu ya AZAKi yetu (programu za AZAKi).	
7.	Wanachama katika AZAKi yetu wanatumia haki yao ya kuuwajibisha uongozi na utawala	
8.	Chombo chetu cha Utawala kinatekeleza kazi zake za kimkakati zikiwemo uandaaji na mapitio ya sera, mikakati na mifumo ya AZAKi	
9.	Muundo wa Bodi yetu umezingatia uwakilishi wa jinsia, wenye ulemavu na makundi mengine ya wadau. Jee, ipo sera ya jinsia inayotilia mkazo ugawaji wa nafasi kwa 50 -50 au vyenginevyo?	
10.	Mwenyekiti wa Bodi au Kamati Tendaji ndiye msemaji wa AZAKi	
	Alama = {a/50 X 30}	

5.0	**Ukweli na Uwazi usio wa kawaida katika utekelezaji wa kazi zetu**	**Max: Alama 20**
1.	AZAKi yetu hutumia vyombo vya habari kukuza utambulisho wake na kazi zake kwa jamii na tunatambulika na vyombo vya habari tofauti kama ni chanzo cha taarifa muhimu kuhusu shughuli tuzifanyazo.	
2.	AZAKi hutayarisha na huwasilisha serikalini, kwa wafadhili na wadau wengine taarifa ya utekelezaji wa kazi na programu zake kwa wakati	
3.	AZAKi kwa kawaida, hutayarisha taarifa za fedha zinazojitosheleza ambazo hujumuisha kazi zetu zote na taarifa hizo hujadiliwa na utawala, uongozi na wadau wengine (wanufaika)	
4.	Wanachama na wanufaika wa AZAKi yetu huhusishwa katika mchakato wa kuchagua na kuweka vipaumbele vya ajenda za ushawishi na utetezi.	
5.	Tunao utambulisho (Alama ya Utambulisho) inayoifanya AZAKi yetu kusimama kifua mbele miongoni mwa wadau wengine (Ainisha utambulisho huu / uhalisia huu)	
6.	AZAKi yetu imeanzisha taratibu zilizo wazi za kuwaelekeza viongozi wetu, wanachama na wafanyakazi kushiriki katika hatua zote za mzunguko wa mradi.	
7.	AZAKi yetu hutumia tulichojifunza kutokana na uzoefu wa utekelezaji wa mradi uliopita kwa ajili ya kuboresha programu zinazofuata.	
	Alama = {a/35 X 20}	

Kumbuka kuambatanisha yafuatayo:

- Maelezo mafupi ya ushuhuda kutoka kwa jamii au kundi lengwa la mradi (maelezo mafupi ya watu angalau wane) waliofaidika na mradi uliofadhiliwa na the Foundation;
- Barua walau mbili kutoka kwa viongozi (wa kijiji au kata, au diwani au kiongozi yeyote wa wilaya au mkoa) ambao watasema kwanini asasi yako inastahili kupewa ushindi katika eneo ulilloomba kushindania.
- Vielelezo vingine kama mkanda wa video, DVD, CD zenye taarifa za mafanikio ya mradi wenu, picha na maelezo yake kuhusu mradi wenu pamoja na nakala za taarifa za kazi zenu zilizochapishwa katika magazeti (newspaper cuts).